# Ufugaji wa Samaki kiafya Tanzania: Kutathmini Changamoto zilozopo na hatua za utatuzi (HATACS project)

## *TAARIFA YA MRADI - Agosti 2024*

Asante kwa kuwa sehemu ya mradi wa HATACS. Hivyo, tungependa tukupatie taarifa za maendeleo ya mradi na hatua zitakazofuata.

### Mradi wa HATACS ni nini?

Ili kutambua njia bora za kusaidia sekta ya ufugaji wa samaki aina ya sato kwa kutumia vizimba katika Ziwa Victoria, mradi wa HATACS uliwaleta pamoja wanataaluma watafiti na wadau muhimu wa sekta ya Tanzania ili:

1. Kutengeneza ramani ya mnyororo wa thamani wa ufugaji wa vizimba wa sato katika Ziwa Victoria,
2. Kujadili fursa, changamoto na suluhisho zinazowezekana katika kudumisha afya ya samaki,
3. Kutambua hatua za kusaidia kuimarisha sekta ya ufugaji wa sato kwa kutumia vizimba nchini Tanzania ili iweze kuendelea kustawi kwa uendelevu

### Ninikimefanyika mpaka sasa?

Shughuli zifuatazo zilifanyika kati ya Aprili 8 hadi 19, 2024:

- Ziara za mashamba na mahojiano ya mtu mmoja mmoja na wafugaji wa sato katika Ziwa Victoria kwa upande wa Mwanza ili kupata uelewa wa changamoto zinazoikabili sekta na fursa zilizopo (8 – 15 Aprili 2024)


- Majadiliano na makundi mawili ya wadau ambayo yalijumuisha wadau muhimu kama wauzaji wa vyakula na vifaranga, wamiliki na wahudumu wa mashamba ya samaki aina ya sato, wasindikaji, wachuuzi, maafisa ugani na wataalam na watafiti kutoka Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI) na National Fish Quality Control Laboratory (NFQCL) ili kujadiliana changamoto na fursa katika mnyoriri wa thamani wa samaki (16-17 Aprili 2024)

- Warsha ya kuainisha vipaumbele vinavyotekelezeka kutoka kwenye mambo ambayo yaliainishwa na kujadiliwa katika majadiliano ya tarehe 16 na 17 Aprili 2024. Warsha hii ilijumuisha baadhi ya washiriki kutoka katika makundi yote mawili ya wadau (18 Aprili 2024)

- Mkutano na wadau kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania (MLF),Umoja wa wafugaji wa Samaki Tanzania (AAT), Halmashauri ya Jiji la Mwanza; NFQCL; na TAFIRI ili kupata maoni ya serikali na sekta, na kujadili changamoto, fursa na vipaumbele vilivyoainishwa wakati wa ziara za mashamba, mahojiano, majadiliano ya makundi na warsha, na kuweka vipaumbele vya suluhisho kwa baadaye pamoja na mahitaji ya utafiti (19 Aprili 2024).

Sokoine University of Agriculture
University of Glasgow
The University of Sydney
University of Stirling

*Shughuli za mradi wa HATACS Mwanza, Aprili 8- 19 2024*




## Tulijifunza nini?

Changamoto zilizoainishwa na wazalishaji, masoko, watoa huduma, wataalamu, wadhibiti, watafiti na wadau wa maabara kama kipaumbele ziligawanywa katika maeneo manne: Mafunzo na kuimarisha Uwezo, upatikanaji na mahitaji ya bidhaa sokoni, Sheria,Udhibiti, na Miundombinu. Maeneo haya yamefafanuliwa zaidi zimefafanuliwa katika jedwali hapa chini, yakiambatana na maoni/mchango kutoka kwa wadau wa serikali pale inapohusika.

**Changamoto za Kipaumbele kwa Hatua**

***1. Mafunzo na kuimarisha Uwezo***

***Changamoto***

- Wakulima hupata mafunzo kwa uchache sana na mara nyingi wanatafuta mbinu binafsi za kutatua changamoto za kiafya zinazowakumba samaki
- Maafisa wa ugani wanatoa usaidizi mzuri, lakini wako wachache ukilinganisha na uhitaji
- Uwezo wa mdogo wa ufuatiliaji wa maji upande wa vizimba hivyo inakua ngumu kufuatilia ubora wa maji na kutabiri pepo zinazovuma ziwani ambazo hupelekea mchafuko mkubwa wa ziwa (*kiferezi*)

***Tatuzi zilizopendekezwa***

- Kuanzisha kituo cha maarifa / kituo cha uchunguzi wa maswala ya majini
- Kuanzisha kituo cha maendeleo kwa ajili ya uzalishaji / mashamba ya vifaranga

**Changamoto za Kipaumbele kwa Hatua**

- Uwezekano wa kuwekeza katika vituo vilivyopo ili mambo yaliyotajwa hapo juu (kwa mfano: TAFIRI, Taasisi ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Wizara)

***Maelezo ya ziada kutoka kwa serikali***

- Kuna nyaraka mbalimbali za mafunzo kuhusu ufugaji wa vizimba lakini vinahitaji kuboreshwa

### 2. *Upatikanaji na mahitaji ya soko*

***Changamoto***

- Upatikanaji wa vifaranga usio wa uhakika (ubora na kiasi), na mara nyingi kutoka katika mazalia yasiyo rasmi
- Upatikanaji wa vyakula vya samaki usio wa uhakika (ubora na kiasi)
- Upendeleo wa watumiaji / dhana potofu kuhusu samaki wa kufugwa dhidi ya samaki wa kuvua ziwani
- Masoko yasiyo ya uhakika / mabadiliko ya bei

***Tatuzi zilizopendekezwa***

- Kutengenezamazingira rafiki ya uwekezaji katika uzalishaji wa vifaranga na chakula cha samaki nchini
- Kuwezesha  upatikanaji wa masoko (la ndani, kitaifa, kimataifa)

***Maelezo ya ziada kutoka kwa serikali***

- TAFIRI ina shamba la mfano  la vifaranga na kiwanda cha chakula cha mfano ili kusaidia kukuza mbinu bora za ufugaji

### 3. *Sheria na Udhibiti*

***Changamoto***

- Mchakato mrefu, mgumu na wenye gharama  wa kibali / leseni
- Sheria na sera tofauti  ambazo mara nyingi zinapingana na zina changamoto za utekelezaji
- Ukosefu wa ulingano katika hatua za kuhakikisha ulinzi wa mashamba dhidi ya vimelea vya magonjwa

***Tatuzi zilizopendekezwa***

- Kituo jumuishi cha huduma kwa ajili ya vibali  naleseni
- uratibu sheria / sera

| Changamoto za Kipaumbele kwa Hatua |
| --- |

- Miongozo ya serikali (& ufuatiliaji / utekelezaji) kwa ajili ya ulinzi wa mashamba dhidi ya vimelea viumbe, ubora wa maji, n.k.

***Maelezo ya ziada kutoka kwa serikali***

- Juhudi zinaendelea kuandaa kanuni za afya ya wanyama wa majini

### 4. *Miundombinu*

***Changamoto***

- Inalazimika kuuza samaki mara tu baada ya kuvuna, hivyo kulazimisha wafugaji kuuza kwa bei ya chini isiyo na tija
- Usafirishaji wa samaki kutoka shambani hadi sokoni unafanyika kupitia barabara mbovu, hali inayoongeza muda wa usafirishaji na kuathiri ubora wa samaki, na hivyo kusababisha bidhaa yenye ubora wa chini

***Tatuzi zilizopendekezwa***

- Utoaji wa vifaa vya kuhifadhi baridi ili kuondoa ulazima wa samaki kuuzwa mara tu wanapovunwa, lakini hata hivyo kutahitajika usambazaji wa umeme wa uhakika kuendesha vifaa hivyo
- Uwekezaji katika barabara bora ili kupunguza muda wa kusafiri kutoka shambani hadi soko na kupunguza uharibifu wa samaki, na hivyo kuongeza ubora

*Ingawa ilikubalika kwamba matatizo ya miundombinu si rahisi kutatuliwa, wadau walionelea kuwa kuna umuhimu wa kuonesha kuwa kuna haja ya Barabara na usambazaji wa umeme kuboreshwa kwa ajili ya vifaa vya kuhifadhi baridi.*

## Nini kinafuata?

Wanataaluma watafiti wanafanya kazi ya kuunganisha matokeo kutoka ziara za mashamba, mahojiano, majadiliano ya makundi na warsha, ili Kuandaa mapendekezo yanayotekelezeka kwa serikali na sekta katika taarifa rasmi iitakayosambazwa kwa wadau kama wewe kwa maoni.

Mara wadau watakapotuambia wanavyoona kuhusu taarifa , tutaipitia tena ili kujumuisha maoni yao na kuihitimisha kwa ajili ya uwasilishaji kwa serikali na sekta.

HATACS ni mradi wa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Chuo Kikuu cha Glasgow, Chuo Kikuu cha Sydney na Chuo Kikuu cha Stirling.

Sekta ya ufugaji wa sato kiafya kwa kutumia vizimba katika eneo la Ziwa Victoria ni muhimu kwa kuhakikisha ustawi endelevu wa ufugaji wa samaki nchini Tanzania.

Sokoine University of Agriculture
UNIVERSITY of GLASGOW
THE UNIVERSITY OF SYDNEY
UNIVERSITY of STIRLING

*The researchers collaborating on this project are Professor Robinson Mdegela, Dr Janeth George (College of Veterinary Medicine and Public Health Sokoine University, Tanzania); Ms Sophia Shaban (Tanzania Fisheries Research Institute); Dr Taya Forde, Dr Angelo Mendes and Professor Cindy Gray (School of Biodiversity, One Health and Veterinary Medicine, School of Social and Political Sciences, The University of Glasgow); Dr Kerrie Wiley and Dr Fransisca Samsing (Sydney School of Public Health, Sydney Veterinary School and Sydney Infectious Diseases Institute, The University of Sydney); Professor Margaret Crumlish (Institute of Aquaculture, The University of Stirling). This project is a collaboration between Sokoine University of Agriculture, Tanzania, The University of Glasgow, The University of Sydney and The University of Stirling. The project is funded through the University of Sydney / University of Glasgow Ignition Grant Scheme, the Glasgow Centre for International Development, and Dr Wiley's University of Sydney Horizons Fellowship.*